Mauti (Kifo) na Ufufuo

“Mshahara wa dhambi ni mauti. Lakini Mungu, ambaye peke yake ana kutokufa, atawapa waliokombolewa wake uzima wa milele. Mpaka siku hiyo mauti ni hali ya kutojifahamu kwa watu wote. Wakati Kristo, ambaye ni uzima wetu, atakapoonekana, wenye hai waliofufuliwa na wenye haki walio hai watabadilishwa na kupewa miili ya utukufu na hivyo kunyakuliwa kwa pamoja na kumlaki Bwana wao. Ufufuo wa pili, ambao ni ufufuo wa waovu, utatokea mika elfu moja baadaye.” (Rum.6:23; 1Tim.6:15, 16; Mhu.9: 5, 6; Zab.146:3, 4; Yoh.11;11-14; Kol.3:4; 1Kor.15:51-54; 1Thes.4:13-17; Yoh.5:28, 29: Ufu.20:1-10)

Jeshi la Wafilisti liliingia Shunem, likaweka kambi na kujiandaa kuipiga Israel. Hali yake ikiwa mbali na ushindi, Mfalme Sauli alipanga Jeshi lake kwenye Mlima Gilboa. Wakati uliopita, uhakika wa uwepo wa Mungu ulimwezesha Sauli kuongoza Israeli dhidi ya maadui yake pasipo hofu. Bali aligeuka akaacha kumtumikia BWANA, na Mfalme mwasi alipojaribu kuulizia kwa BWANA juu ya matokeo ya vita, Mungu alikataa kuwasiliana naye.

Hofu korofi ya matokeo ya vita yasiyojulikana ilimwelemea Sauli kwa uzito. Kama Samweli angekuwako hapa. Lakini Samweli alikuwa amekufa na asingeweza kumshauri. Au angeweza? Akitambua aliko mchawi aliyeokoka katika misako yake iliyopita, Mfalme mrefu aliinama kuulizia matokeo ya vita itakayopiganwa kesho. Aliomba, “Nipandishie Samweli.” Katika tukio hilo, mwanamke aliona “roho akipanda kutoka kwenye nchi”. Huyu ‘roho’ alimwambia Mfalme mwovu kuwa siyo tu Israeli watashindwa vita ila pia, yeye na mwanae watakufa vitani. (1Samweli 28).

Utabiri uliotolewa ulitimia. Je, hivi ni kweli roho ya Samweli ndiyo iliyotoa unabii? Inawezekanaje, mchawi anayelaumiwa na Mungu awe na nguvu kwenye ‘*roho*’ ya Samweli – nabii wa Mungu? Ni wapi Samweli alikotokea, katika nchi? Kifo kilikuwa kimemtendea nini Samweli? Kama siyo roho ya Samweli iliyoongea na Sauli, ni nani basi? Hebu tutazame jinsi Biblia inavyofundisha juu ya kifo, kuwasiliana na wafu na ufufuo.

Hali ya Kutokufa na Mauti (Kifo)

Kutokufa ni hali au ubora wa kutofikiwa na kifo. Watafsiri wa Maandiko walitumia neno kutokufa kutafsiri neno la Kigiriki *athanasia* “kutokufikwa na kifo – deathlessness” *aphtharsia* “kutokuharibika”. Je, mambo haya yanahusika vipi na mwanadamu?

Kutokufa. Maandiko Matakatifu hufunua kwamba Mungu wa milele ana hali ya kutokufa. (1Tim.1:17). Kwa kweli, Yeye peke yake ana hali ya kutokufa. (1Tim.6:16). Hakuumbwa, anaishi mwenyewe pasipo kuwezeshwa na hana mwanzo wala mwisho. (Angalia somo la Utatu Mtakatifu).

Hakuna mahali popote katika Maandiko ambako kutokufa inatajwa kuwa hali ambayo mwanadamu anayo, au nafsi yake, au roho yake inayo. Maneno nafsi na roho hupatikana kwenye Biblia zaidi ya mara 1600 na kote hakuna ambako maneno husika yameambatana na hali ya kutokufa au kutokuharibika. (Angalia somo la Mwanadamu na Asili Yake).

Tofauti na Mungu, mwanadamu ana hali ya kufa. Maandiko hulinganisha hali hiyo na “mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka. (Yak.4:14). Ni ‘kiwiliwili, upepo upitao

wala haurudi." (Zab.78:39). Mwanadamu "huchanua kama vile ua, kisha hukatwa; hukimbia kama kivuli, wala hakai kamwe. (Ayu.14:2). Mungu na mwanadamu hutofautiana sana. Mungu hana mwisho, mwanadamu ana ukomo. Mungu hapatikani na mauti, mwanadamu hufa. Mungu ni wa milele, mwanadamu ni wa kupita.

Hali ya Kutokufa yenye Masharti. Katika Uumbaji, Mungu alimfanya "mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai." (Mwa.2:7). Habari ya uumbaji hudhihirisha kuwa mwanadamu alipata uhai wake kutoka kwa Mungu. (cf. Mdo.17:25, 28; Kol.1:16, 17). Ukweli unaoonekana kwa maelezo haya ni kwamba kutokufa yaani uzima wa milele siyo hali aliyo nayo mwanadamu bali ni karama ya Mungu. (Rum.6:23).

Mungu alipowaumba Adamu na Hawa, aliwapa uhuru wa kuchagua. Wangeweza kuchagua kutii au kutokutii, lakini kuendelea kuwa hai, kulitegemea utii unaoendelea kupitia uwezo wa Mungu. Kwa hiyo, kuwa kwao na kutokufa (uzima wa milele), kulitegemea kutimiza masharti. Mungu kwa uangalifu mkubwa, alitaja masharti husika. "Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakayokula matunda ya mti huo utakufa hakika." (Mwa.2:17).

Mauti (Kifo) Mshahara wa Dhambi. Akipinga onyo la Mungu kwamba kutokutii kutaleta kifo, Shetani alidai "Hakika hamtakufa." (Mwa. 3:4). Lakini baada ya kutokutii, Adamu na Hawa waligundua kuwa mshahara wa dhambi kwa uhalisi ni "mauti" (Rum.6:23). Hukumu yao ilibeba maneno haya: "kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi."(Mwa.3:19).

Baada ya hukumu, Mungu alizuilia wanandoa wenye dhambi wasiufikie Mti wa Uzima wasije wakala matunda yake na kuishi milele. (Mwa.3:22). Kitendo chake kiliweka wazi kwamba kutokufa ambako kuliahidiwa kutokana na utii kulipotea kwa sababu ya dhambi. Sasa wamekuwa watu wenye hali ya kufa, na kwamba watakufa. Kwa sababu Adamu asingeweza kurithisha uzao wake hali ambayo hana, "hivyo mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi." (Rum.5:12).

Ni rehema ya Mungu tu ndiyo iliyowafanya Adamu na Hawa wasife mara moja baada ya dhambi. Mwana wa Mungu alikuwa amejitolea kutoa uhai wake ili kwamba mwanadamu awe na fursa nyingine. Yeye ni "Mwanakondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia." (Uf. 13: 8).

Tumaini kwa Mwanadamu. Pamoja na kwamba wanadamu huzaliwa wakiwa na hali ya kufa, Biblia huhimiza watafute kutokufa. (Angalia kwa mfano Rum. 2:7). Yesu Kristo ndiye chanzo cha kutokufa. "Bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." (Rum. 6:23 cf. 1Yoh. 5:11). Kristo Yesu alibatili mauti na kufunua uzima na kutokuharibika. (2Tim.1:10)."Kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa." (1Kor.15:22). Kristo mwenyewe alisema sauti yake itafungua makaburi na kufufua wafu. (Yoh.5:28, 29).

Kama Kristo asingelikuja, hali ya mwanadamu ingekosa matumaini na waliokufa wangepotea milele. (Yoh.3:16). Kwa hiyo, imani kwa Kristo siyo tu inamwepushia mwanadamu adhabu ya kifo ila pia inampatia zawadi yenye thamani kuu ya kutokufa.

Kristo alituletea kutokufa kupitia nuru ya injili. (2Tim.1:10). Paulo anathibitisha kwamba Maandiko Matakatifu yaweza kutuhekimisha hata kupata uzima wa milele. (2Tim.3:15). Wanaoikataa injili, hawatapokea kutokufa.

Kupokea kutokufa. Wakati wa kupokea kutokufa umesimuliwa na Paulo. "Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatulala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa. Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda." (1Kor.15:51-54). Hii huweka wazi kuwa Mungu hatatupatii kutokufa wakati tunapokufa, badala yake atatupatia kutokufa wakati parapanda itakapolia, ndipo mwili wa kufa, utapovaa kutokufa. Ni kweli Yohana husema kwamba tunapompokea Yesu tunapata uzima wa milele (1Yoh.5;11-13). Utimilifu wa kupokea uzima wa milele utatokea siku Yesu akirejea mara ya pili. Hapo ndipo tutabadilishwa kutoka wa kufa kuwa wa kutokufa na wa kuharibika kuwa wa kutokuharibika.

Asili ya Mauti (Kifo)
Ikiwa mauti ni kukoma kuwa uhai (uzima), Biblia inasemaje kuhusu hali ya mtu aliyekufa? Kuna umuhimu gani kwa wakristo kufahamu jambo hili?.

Mauti (Kifo) ni usingizi. Mauti (kifo) siyo maangamizi kamili bali ni hali ya kutokuwa na fahamu kwa muda wakati mtu anasubiri ufufuo. Biblia kwa kurudia rudia huiita hali hiyo usingizi.

Likielezea vifo vya wafalme wa Israeli, Agano la Kale linasema kifo cha Daudi, Sulemani, na wafalme wengine na Yuda kuwa wamelala na baba zao. (1Fal.2:10; 11:43; 14:20, 31; 15:8; 2Nyak.21:1; 26:23; nk.). Ayubu alikiita kifo usingizi (Ayu. 14:10-12), kama Daudi (Zab.13:3) Yeremia (Yer.51:39, 57) na Danieli (Dan. 12:2). Agano Jipya hutumia msemo huo pia. Akielezea hali ya binti Yairo ambaye alikuwa amekufa, Kristo alisema kuwa amelala (Mt. 9:24; Mk.5:39). Alimwelezea Lazaro aliyekufa kwa namna hiyo hiyo (Yoh.11:11-14). Mathayo aliandika, "ikainuka miili mingi ya watakatifu waliolala" (Mt.27:52) wakitoka makaburini mwao baada ya kufufuka (Mt.27:53). Akielezea kuuawa Stefano, Luka aliandika akisha kusema haya, "akalala". (Luk.7:60). Paulo na Petro pia walikiita kifo usingizi. (1Kor. 15:51, 52; 1Thes.4:13-17; 2Pet.3:4).

Kwa nini usingizi ni kielelezo kizuri kuelezea kifo? Maelezo ya Biblia kama usingizi yanafaa kwa asili yake kwa kuwa kuna kufanana kwa kifo na usingizi. 1. Waliolala hawana ufahamu. "lakini wafu hawajui neno lolote" (Mh.9:5). Katika usingizi, hakuna kufikiri. "Pumzi yake hutoka… siku hiyo mawazo yake yapotea" (Zab.146:4) 3. Usingizi huwa ukomo wa kazi za siku. "kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe" (Mhu. 9:10). 4. Usingizi hututenga na walio macho na matendo yao. "Wala hawana sehemu tena katika jambo lolote lililofanyika chini ya jua." (Mhu.9:6). 5. Usingizi wa kawaida hufanya hisia kutokutenda kazi. "Mapenzi yao, na machukio yao, na husuda yao imepoa yote pamoja. (Mhu.9:6). 6. Kwenye usingizi, watu hawawezi kumsifu BWANA. "Sio wafu wamsifuo BWANA, wala wowote washukao kwenye kimya." 7. Usingizi hutangulia kabla ya

kuamka. “”saa yaja ambayo waliomo makaburini wataisikia sauti yake; nao watatoka." (Yoh. 5:28,29)

Mtu kurudi Mavumbini. Kuelewa kinachotokea mtu akifa, twapaswa kuelewa kinachomfanya binadamu. (Angalia somo la Mwanadamu na Asili yake). Kwenye uumbaji wa mwanadamu, mwungano wa mavumbi ya ardhi (udongo) na pumzi ya uhai vilimfanya nafsi hai (Mwa.2:7). Katika kifo, kinyume chake hutokea: mavumbi ya ardhi yakiondolewa pumzi ya huai hufanya mfu asiye na ufahamu (Zab.146:4). Yaliyomtengeneza mwanadamu hurudi yalikotoka. (Mwa.3:19). Roho haina uhai nje ya mwili, wala hakuna andiko linalodokeza kuwa katika mauti nafsi (ambayo huitwa roho) huishi kama kitu hai. Kwa ukweli, “roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa.” (Eze.18:20).

Wafu wako wapi? Agano la Kale linapaita mahali walipo wafu kuwa ni *sheol* (Kiebrania) na Agano Jipya *hades* (Kigiriki). Katika Maandiko, maana rahisi ya *sheol* (kuzimu) ni kaburi. Maana ya *hades* ni sawa na maana ya *sheol*.

Wafu wote huenda mahali hapo. (Zab.89:48), wema kwa waovu. Yakobo alisema atamshukia mwanawe hata kuzimu (Mwa.37:35). Ardhi ilipofunguka, iliwameza Kora pamoja na wenzake hadi kwenye *sheol* (Hes.16:30). *Sheol* hupokea mtu mzima. Kristo alipokufa, alizikwa kaburini (hades) lakini katika Ufufuo, nafsi yake iliacha kaburi hades (Mdo.2:27, 31) au sheol. (Zab.16:10). Daudi alipomshukuru Mungu kwa uponyaji, anashuhudia kuwa aliokolewa kutoka kwenye *sheol* (kuzimu/kaburi). Kaburi siyo mahali pa ufahamu. Kwa kuwa kifo / mauti ni usingizi, wafu watabaki pasipo kuwa na ufahamu hadi hades (kuzimu) kutakapotoa wafu wake. (Uf.20:13).

Roho kumrudia Mungu. Ijapokuwa mwili hurudi udongoni, roho humrudia Mungu. (Mh.12:7). Hili ni jambo linalotokea kwa wote, wema kwa waovu. Wengi wamedhani kwamba fungu hili la Biblia huhakikisha kwamba kipo kipengele ndani ya mwanadamu kinachoendelea kuishi baada ya kufariki. Lakini katika Biblia, neno *roho (*Kwa Kiebrania *ruach* au Kigiriki *pneuma*), haimaanishi kitu kizima chenye akili kinachoweza kuishi peke yake pasipo mwili. (Angalia somo la Mwanadamu na Asili yake). Kufuatana na Sulemani, katika kifo, hakuna tofauti ya roho za wanyama na za wanadamu, wote huenda pamoja. (Mh.3:19-
21). Anachomaanisha kuwa kinamrudia Mungu ni ile kanuni, cheche ya uhai. (Mwa.2:7).

Kupatana kwa Maandiko. Watu waaminifu ambao hawajajifunza kwa makini Biblia, hawajafahamu kwamba kifo ni usingizi hadi mtu atakapofufuliwa. Wanadhani kwamba yako mafungu yanayohakikisha wazo la mtu kuwa na hali nyingine ya uhai. Kujifunza kwa makini huhitimisha kwamba kifo hufanya kukoma kwa ufahamu (uhai).

Imani ya Kuongea na Wafu (Spritualism). Ikiwa wafu hawana ufahamu, je, wanaongea na wafu huwa wanaongea na nani? Kila aliye mwaminifu atakubali kwamba baadhi ya matukio yanayodaiwa kwamba wafu wanaongea, ni ya hila. Lakini mengine hayana maelezo. Kuna nguvu zinazopita nguvu za asili isiyo ya kawaida iliyoungana na imani ya kuongea na wafu. Biblia hutufundisha nini kuhusiana na jambo hili?

1. Msingi wa Imani ya Kuongea na Mizimu (Wafu). Imani ya kuongea na wafu imeanzia kwenye uongo wa awali wa Shetani kwa Hawa. “Hakika hamtakufa” (Mwa.3:40). Maneno

hayo yalikuwa hubiri la kwanza juu ya kutokufa kwa roho (nafsi). Katika ulimwengu wa leo, ziko jamii nyingi za kidini zinazorudia kosa hilo.
Kwa wengi, ile hukumu kwamba roho itendayo dhambi itakufa (Eze.18:20) imebadilishwa na kuwa “roho hata ikitenda dhambi itaendelea kuishi milele.”

Imani ya kwamba watu waliokufa wana fahamu, imewaandaa Wakristo wengi kukubali imani ya kuongea na mizimu. Kwa kutumia uwongo huo, Shetani na malaika zake (Ufu.12:4, 9) wameanzisha namna ya mawasiliano na wafu. Wakati mwingine hutoa utabiri, na utabiri huo unapotimia, huanza kuaminika kwenye jamii. Ndipo uwongo wake unapohesabika ni jambo la hakika hata kama unapingana na Biblia au Sheria ya Mungu. Kwa kuondosha kizuizi cha uovu, Shetani anao utawala huru unaoongoza wanadamu mbali na Mungu na kwenye uharibifu wa hakika.

2. Onyo dhidi ya Imani ya Kuongea na Mizimu. Hakuna moja apaswaye kudanganywa na imani ya kuongea na wafu. Biblia kwa uwazi hufunua kwamba madai yake ni uwongo. Kama tunavyojua, tayari Biblia inatuambia kwamba wafu hawajui lolote na kwamba wako makaburini pasipo na ufahamu.

Biblia pia hukataza jaribio lolote la kuwasiliana na wafu au roho za kidunia. Husema wote ambao hudai kuwasiliana na wafu kwa uhalisi huwa wanawasiliana na pepo wachafu au roho za mashetani. Bwana asema vitendo hivyo ni machukizo na wowote ambao wangehusika navyo walipaswa kuadhibiwa kifo. (Law.19:31; 20:27 cf. Kumb.18:10, 11). Isaya anaelezea vema upumbavu wa imani ya kuongea na wafu. “Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong’ona; je! Haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao pana asubuhi”. (Isa.8:19, 20). Kwa hakika, ni mafundisho ya Biblia tu ndiyo yatakalinda Waksristo dhidi ya uwongo huu wa kutisha.

3. Matukio Yanayojitokeza ya Imani ya Kuongea na Wafu. Biblia inayo kumbukumbu za imani ya kuongea na wafu – kutokea kwa wachawi wa Farao na wachawi, waganga na wasihiri wa Ninawi na Babeli na wachawi na waaguzi wa Israeli na kuwahukumu wote hao. Biblia inasema: “Lakini Sauli alipouliza kwa BWANA, BWANA hakumjibu, wala kwa ndoto, wala kwa Urimu, wala kwa manabii.” (1Sam.28:6). Kwa hiyo, Mungu hakuwa na sehemu ya kilichotokea Endori. Sauli alidanganywa na pepo lililojifanya nabii Samweli; kamwe hakumwona Samweli halisi. Alichoona mchawi kilikuwa umbo la mzee wakati Sauli alihihesabu na kuhitimisha kwamba ni Samweli. (1Sam.28:14).

Ikiwa tutaamini kwamba kilichoonekana ni Samweli, lazima tujiandae kuamini kwamba wachawi, wasihiri, waganga, wanajimu, wapiga bao wanaweza kuwaita watakatifu waliokufa popote walipo baada ya kufa. Pia lazima tuamini kwamba Samweli wa Mungu aliishi akiwa na ufahamu ndani ya nchi, kwa sababu mwanaume mzee aliinuka “kutoka kwenye nchi.” (fungu la 13).

Mazungumzo yaliyofanyika yalimkatisha tama Sauli wala hayakumpa tumaini. Siku iliyofuata, alijiua. ((1Sam.28:19). Kama angekuwa sahihi, tungehitimisha kwamba baada ya

kufa, Sauli mkaidi na Samweli mwenye haki waliishi pamoja. Badala yake inatulazimu kuhitimisha kwamba malaika mwovu alileta matukio ya kudanganya katika mazingira haya.

4. Udanganyifu wa mwisho. Wakati uliopita, matukio yaliyojitokeza ya Imani ya Kuongea na Wafu yalijibana kwenye ulimwengu wa uchawi, lakini siku hizi, imaini ya kuongea na wafu inabeba taswira ya "Kikristo" ili idanganye ulimwengu wa kikristo. Kwa kukiri kumkubali Yesu na Biblia, Imani ya Kuongea na Wafu (mizimu) imekuwa adui wa hatari kwa waumini.Matokeo yake ni ya pole pole na yanadanganya. Kupitia imani hiyo, Biblia hutafsiriwa kwa namna ambayo hupendeza moyo usiofanywa upya, wakati maonyo na ukweli muhimu yakifanywa hayana athari yoyote. Upendo unakuwa tabia kuu ya Mungu, lakini huhafifishwa kwa mambo ya hisia, ikiwekwa tofauti ndogo baina ya mema na mabaya. Hukumu ya Mungu, chuki yake kwa dhambi, madai ya sheria yake takatifu yanaepukwa. Watu wanafundishwa kutazama amri kumi kama iliyo ya maana. Hadithi za kichawi chawi, huteka fikra na kuwangoza watu kuikataa Biblia kama msingi wa imani yao.

Kupitia njia hiyo, mema na mabaya yanafanywa kuhusiana, na kila mtu au hali, au utamaduni unakuwa kanuni ambayo ni kanuni ya kuishi kwayo ya kile kinachohesabika kuwa ni "kweli." Kwa uhalisi, kila mtu anakuwa mungu, akitimiza ahadi ya Shetani kwamba "mtakuwa kama miungu" (Mwa.3:5).

Mbele yetu iko "saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi." (Ufu.3:10). Karibu, Shetani atatumia miujiza mikubwa na maajabu katika juhudi yake ya mwisho kuudanganya ulimwengu. Akizungumzia jambo hili, nabii Yohana anasema "Naliona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uwongo. Hizo ndizo roho za mashetani zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mwenyezi Mungu." (Ufu.16:13, 14 cf. 13:13, 14).

Ni wale tu wanaolindwa na uwezo wa Mungu, mawazo yao yakijikita kwenye kweli ya Maandiko Matakatifu, wakiyakubali kwamba ndiyo mamlaka pekee, wataweza kuokoka. Wengine wote hawana ulinzi nao watazolewa na uwongo huu.

Mauti ya Kwanza na Mauti ya Pili. Mauti ya pili ni adhabu ya mwisho ya wenye dhambi wasiotubu – wote ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha uzima - itakayotolewa baada ya miaka 1,000 (Angalia somo la Miaka Elfu). Kwa mauti ya pili hakuna ufufuo. Kwa maangamizi ya Shetani na wasio haki, dhambi inaondoshwa, na kifo chenyewe kinaharibiwa. (1Kor. 15:26; Ufu.20:14; 21:8). Kristo ametuhakikishia kwamba "yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili. (Ufu.2:11). Kwa msingi wa Maandiko kwamba mauti ya pili ni adhabu kwa dhambi, twaweza kuhesabu kwamba mauti ya kwanza ni ile impatayo kila mwanadamu isipokuwa wale ambao watakuja kubadilishwa siku Yesu akirudi, uzoefu tulioupokea kutoka uasi wa Adamu. Ni kawaida inayotokana na kuendelea kuharibika kwa sababu ya dhambi.

Ufufuo

Ufufuo ni kurejeshewa uhai, pamoja na ukamilifu wa kuwapo na nafsi, baada ya kufa. Kwa kuwa wanadamu hupatwa na mauti, lazima uwepo ufufuo ikiwa watakuwa na uhazi baada ya kaburi. Kwenye Agano la Kale na Agano Jipya, wajumbe wa Mungu walieleza tumaini lao kwa ufufuo. (Ayu.14:13-15; 19:25-29; Zab.49:15; 73:24; Isa.26:19; 1Kor.15). Tumaini la

ufufuo ambalo tunao ushahidi wake wa kutosha, hututia shime kutazamia maisha bora ng'ambo ya ulimwengu wa sasa, ambako sote twakabiliwa na kifo.

Ufufuo wa Kristo. Ufufuo wa wenye haki waliokufa kuvaa kutokufa unafanana kwa karibu na ufufo wa Kristo, kwa sababu ni Kristo aliyefufuka ndiye hatimaye atafufua wafu. (Yoh.5:28, 29).

1. Umuhimu wake. Nini kingetokea ikiwa Kristo asingekuwa amefufuka? Paulo anafanya mhutasari wa matokeo: a. kusingekuwa na maana kuihubiri injili. "tena kama Kristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure." B. Kusingekuwa na msamaha wa dhambi: "na kama Kristo hakufufuka…mngalimo katika dhambi zenu. (fungu la 17). c. Kusingekuwa na maana kumwamini Yesu. "Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure." d. Kusingekuwa na kufufuliwa wafu. "Basi, ikiwa Kristo anahubiriwa ya kwamba amefufuka katika wafu, mbona baadhi yenu husema hakuna kiyama ya wafu?" (fungu la 12). e. Kusingekuwa na tumaini ng'ambo ya kaburi. "Ikiwa Kristo hakufufuka…na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea." (1kor.15:17, 18).

2. Ufufuo wa mwili. Kristo aliyetoka kaburini alikuwa Yesu yuleyule aliyeishi hapa katika mwili. Sasa ana mwili uliovikwa utukufu, lakini bado ni mwili ule ule. Ulikuwa mwili halisi kiasi ambacho wengine hawakuona tofauti.(Luk.24:13-27; Yoh.20:14-18). Yesu mwenyewe alikana kwamba siyo roho au pepo. Akiongea na wanafunzi wake, alisema: "Tazameni mkono yangu na miguu yangu, ya kuwa mimi ni mwenyewe" (Luk.24:39). Kuthibitisha kwamba ana umbo halisi baada ya kufufuka, pia alikula pamoja nao. (fungu la 43).

3. Athari yake. Ufufuo ulikuwa na athari ya kuwasisimua wanafunzi. Ulibadili kikundi cha watu wanyonge na waoga kuwa mitume mashujaa wakiwa tayari kufanya lolote kwa ajili ya Bwana wao. (Fil.3:10, 11; Mdo. 4:33). Utume walioufanya yakiwa matokeo ya ufufuo, ulitikisa dola ya Rumi na ukapindua ulimwengu. (Mdo.17:6).

Ilikuwa ni uhakika wa kufufuka kwa Kristo ndio ulioleta hoja na uwezo wa kuhubiri injili. (cf. Fil.3:10, 11). Petro anazungumzia ufufuo wa Yesu kuwa ulileta tumaini la uzima (1Pet.1:3). Mitume walijihesabu kwamba wamewekwa wakfu kuhubiri ufufuo. (Mdo.1:22), na mahubiri yao yalikuwa kwenye msingi kuwa ufufuo wa Yesu wa Masihi ulitabiriwa (Mdo.2:31). Ilikuwa ufahamu wao binafsi kuhusu ufufuo kulikowapa uwezo wa kushuhudia kwa nguvu kufufuka kwa Yesu. (Mdo.4:33). Mitume walivutia upinzani wa Viongozi wa Kiyahudi walipofundisha watu na kuhubiri katika Yesu ufufuo wa wafu. (Mdo.4:2). Aliposhtakiwa mbele ya Baraza la Wayahudi (Sanhedrin), Paulo alipaza sauti kwamba ni kwa sababu ya tumaini lake la ufufuo wa wafu kwamba anahukumiwa. (Mdo.23:6; cf. 24:21). Kwa Warumi, Paulo aliandika kamba Yesu Kristo ali "dhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu … kwa ufufuo wa wafu." (Rum.1:4). Kwenye ubatizo, alieleza Mkristo anakiri imani yake katika ufufuo wa Kristo. (Rum.6:4, 5).

Fufuo Mbili. Kristo alifundisha kwamba kwa ujumla ziko fufuo mbili: "ufufuo wa uzima" kwa wenye haki na "ufufuo wa hukumu" kwa wasio haki. (Yoh.5:28, 29; Mdo. 24:15). Miaka 1,000 inatenganisha fufuo mbili hizi. (Ufu.20:4, 5).

1. Ufufuo wa uzima. Wanaofufuliwa kwenye ufufo wa kwanza wameitwa "heri na mtakatifu" (Ufu.20:6). Hawatapata mauti ya pili katika ziwa la moto mwisho wa miaka 1,000.

(Ufu.20:14). Ufufuo wa uzima na kutokufa (Yoh.5:29; 1Kor.15:52, 53) utafanyika Yesu akija mara ya pili. (1Kor.15:22, 23; 1Thes.4:15-18). Wale watakaopata ufufuo huu hawatakufa tena. (Luk.20:36). Wataungana na Kristo milele.

Mwili uliofufuliwa utakuwaje? Kama Kristo mfufuka alivyokuwa, watakatifu watakuwa na miili halisi. Na kama Kristo alivyofufuka, mwenye utukufu, ndivyo watakatifu watakavyokuwa. Paulo alisema kwamba Kristo ataubadili "mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu." (Filp. 3:21). Anauita mwili wa sasa kuwa usio na utukufu na wa kuharibika na ule wa ufufuo kuwa mwili wenye utukufu na mwili wa kiroho; wa kwanza kuwa wenye kufa na kuharibika na wa pili usiokufa wala usioharibika. Badiliko kutoka kufa kwenda kutokufa litafanyika kwa kufumba na kufumbua katika ufufuo. (1Kor.15:42-54).

2. Ufufuo wa hukumu. Wasio haki watafufuliwa kwenye ufufuo wa kiujumla wa pili, utakaofanyika baada ya miaka1,000. (Angalia somo la Miaka 1,000). Ufufuo huu unaendelea kwenye hukumu ya mwisho na waovu kuadhibiwa. (Yoh.5:29). Ambao majina yao hayamo kwenye Kitabu cha Uzima watafufuliwa wakati huo na "kutupwa kwenye ziwa la moto" na kupokea mauti ya pili. (Ufu.20:14, 15).

Wangeweza kuepuka mwisho mbaya wa namna hii. Kwa lugha isiyokosewa, Maandiko Matakatifu huwakilisha njia ya Mungu ya kuoka. "Rudini, mkaghairi, na kuyaacha makosa yenu yote; basi hivyo uovu wenu hautakuwa uharibifu wenu. Tupilieni mbali nanyi makosa yenu yote mliyoyakosa; jifanyieni moyo mpya na roho mpya; mbona mnataka kufa enyi nyumba ya Israel? Maana mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana MUNGU; basi ghairini mkaishi." (Eze.18:30-32).

Kristo anaahidi kwamba "yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili. (Ufu.2:11). Watakaomkubali Yesu na wokovu anaouleta watapata furaha isiyo kifani siku akirudi kwa kishindo. Katika furaha isiyofifia, watatumia umilele wakiwa washirika wa Bwana na Mwokozi wao.

===Mwisho wa somo====

Mafungu ya Biblia yanayodhaniwa Kuelezea Wafu wako Hai
Yapo mafungu katika Biblia ambayo hutafsiriwa vibaya hata kudhania wafu wana hali ya kutokufa na hivyo wanadamu walio hai wanaweza kufanya maombi, au kutekeleza sharti la mhubiri wa injili ili hao waliokufa warejee kwenye hali ya mwili unaoonekana tena. Mafungu husika yameonyeshwa na kupewa maelezo yake.

Maelezo ya Mafungu
1. Mwa. 35:18 "Ikawa hapo katika kutoa roho yake" Hii ina maana katika nyakati za pumzi ya mwisho za uhai wake alimwita mtoto Benoni.
2. 1Fal.17:21, 22 "Nakusihi roho ya mtoto huyu imrudie ndani yake" Mungu alipojibu ombi hili kwa kumfufua mtoto wa mwanamke wa Sarepta, kanuni ya uhai ilitumika. Siyo mwili wala roho iliyokuwa na uhai peke yake, bali vilipoungana, mtoto alifufuka.
3. Kuonekana kwa Musa kwenye mlima aliobadilika Yesu. (Mt.16:28-17:3). Yesu alikuwa ameahidi baadhi ya wanafunzi wake hawatakufa hadi wamwone katika utukufu. Na hapo,

fursa ndogo ilitolewa kwa Petro, Yohana na Yakobo. Kwenye mlima, alitokea Musa aliyekufa zamani (Kumb.34:5, 6) na Eliya aliyepaa (2Fal.2:11). Musa na Eliya wanawakilisha jamii ya wanadamu watakaobadilishwa kuurithi ufalme wa milele. Kwamba wapo watakaokufa kabla ya kufufuliwa na kubadilishwa na wapo watakaobadilishwa pasipo kufa na kunyakuliwa. Yuda ana ushahidi kwamba Musa alifufuliwa kwenye ufufuo wa pekee (Yud. 9). Baada ya Mikaeli kushindana na Ibilisi, Ibilisi alishindwa na Musa akafufuliwa. Ufufuo wa Musa, hauungi mkono kutokufa kwa roho bali ufufuo wa mwili.

4. Kuishi ni Kristo na kufa ni faida… ninasongwa katika mambo mawili, ninatamani nikakae na Kristo maana ni vizuri sana. (Filp.1:21, 23). Je, Paulo alitegemea kuingia mbinguni mara moja baada ya kufa kwake? Hapana. Paulo amezungumzia somo la wafu kwa upana wake. Kwenye waraka mwingine aliandika "waliokufa katika Kristo", katika ujio wa Kristo watafufuliwa kwanza. (1Thes.4:16). Ndipo walio hai na waliofufuliwa watanyakuliwa ili kumlaki Bwana hewani. (fungu la 17). Na kwamba ni nafsi, mwili na roho ndivyo vitakavyokuwa na Kristo (1 Thes. 5: 23).
5. 1 Pet. 3: 18-20 na 4:6 Petro anaposema kuwa Yesu alikwenda kuhubiri walio kifungoni, ieleweke kuwa dunia yote inahesabika iko kuzimu cf Mt. 11:23. Biblia hufundisha wokovu hutafutwa wanadamu wakiwa hai, siyo wakishakufa.
6. Ebr. 11: 4, Habili atanenaje wakati akiwa marehemu? Ni kwamba matendo yake aliyotenda akiwa hai, yaani kutoa sadaka zinazokubalika kwa Mungu, hata kama amekufa, yameacha kielelezo ambacho kinafundisha walio hai.
7. Ufunuo 6: 9 – 11 Yohana alikuwa anaona sinema yenye fundisho la kiroho. Hakuwa anatazama mbinguni jinsi ilivyo kwa uhalisi. Kanuni za kutafsiri Ufunuo haitupatii sisi wasomaji mamlaka ya kujitungia tafsiri zetu (2 Pet. 1: 20) Kinachosemwa hapa ni kwamba mtazamo unabadilika kutoka uangamivu na vifo ambavyo watakatifu hukabiliana navyo hadi kwenye wanachostahili watakatifu wenyewe.

   Luka 23: 43 Yesu alipokufa, hakupaa mbinguni moja kwa moja. Alibaki duniani baada ya kufufuka kwa siku kadha wa kadha. Siku ya kwenda mbinguni, alipaa peke yake wingu akiwa mtu moja, hakuna maelezo kuwa mwizi aliyeungama alikwenda naye. (Mdo. 1: 9-11). Hivyo, kinachosemwa na fungu ni kuwa ahadi ya uzima ilitolewa siku ile wakiwa wote msalabani.

Kisa cha Tajiri (mara nyingi huitwa Dives) na maskini Lazaro (*Luk. 16: 19 – 31)*

Wayahudi walikuwa na utaratibu wa kutumia mifano kwenye simulizi zao. Kwa mfano, katika Waamuzi 9:7-15 ikilinganishwa na 2 Wafalme14:9, utasoma miti inaongea. Hakuna mtu atakayetumia mafungu ya mifano hiyo kuthibitisha kwamba miti huongea. Mfano wa Tajiri na Maskini Lazaro ulikuwa mfano maarufu wa wafu wanaoongea nyakati za Yesu. Kisa ni miongoni mwa mifano iliyotolewa kuwalenga mafarisayo (Luk. 15:2). Mafarisayo walipomwona Yesu anakula na kunywa pamoja na walio na dhambi, walinung'unika, Mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi na kula nao. Hivyo Yesu akawapa mifano ya kondoo aliyepotea, shilingi iliyopotea na Baba mwenye watoto wawili (wengine mnakiita kisa cha mwana mpotevu). Lengo la Yesu lilikuwa kuwaonyesha mafarisayo upendo wa Mungu kwa mwenye dhambi. Na ndiyo maana alisisitiza kuna furaha mbinguni kwa mwenye dhambi atubuye. (Luka 15: 7, 10)

Baada ya hayo akafundisha wanafunzi wake, juu ya uwakili. (Luk. 16: 1-13). Alipomaliza, mafarisayo waliokuwa wanasikiliza alichokuwa anafundisha wanafunzi wake walimdhihaki. Mafarisayo hao walikuwa wakiamini maskini ni maskini kwa sababu wamelaaniwa na matajiri ni matajiri kwa sababu wamebarikiwa. Na kwa hiyo, kule kuwa maskini ilihesabika katika jamii kuwa ni mapigo ya Mungu kwa mwanadamu mwenye dhambi. Na utajiri ilikuwa ni alama ya kubarikiwa na Mungu. Wakati watu wa kawaida walifurahia mafundisho ya Yesu (Mk. 12:37), mafarisayo walikuwa wakikasirika (Luk. 15:2). Na kwa mafarisayo, Yesu alikuwa na ujumbe kuwa Ole wenu... wanafiki kwa kuwa mnaufunga mlango wa ufalme wa mbinguni, ninyi wenyewe

hamuingii na mnawazuia wanaotaka kuingia (Mt. 23:13). Dhihaka ya mafarisayo Luk. 16:14 -18 ilifanya mfano wa Tajiri na maskini Lazaro utolewe. Maelezo ya Hukumu itakavyokuwa ni kwamba:

1. *Biblia hufundisha kuwa maamuzi kwa ajili ya kuokolewa hufanyika mtu akiwa hai na kwamba rehema hufungwa mtu akifa*

   Mt. 16:27 Mtu atalipwa kadiri ya matendo yake

   Luk. 16: 26-31 Ombi la tajiri kurudi kuonya walio hai lilikataliwa kwamba walio hai wasikilize ya Musa na Manabii

   Rum. 2:6 kila mtu alipwa kwa kadiri ya matendo yake

   Ebr. 9: 27 Baada ya kifo hukumu (Zingatia: hukumu ni tamko la ijara siyo utekelezaji)

   Uf. 22:12 Ijara itatolewa Yesu atakapokuja

   Yesu mwenyewe alifundisha ijara ya watakatifu na ijara ya waovu. Ijara ya Watakatifu : Peponi (Luk. 23:43), Ufalme wa baba (Mt. 26:29), Mbinguni (Mt. 6:20), Makao na Baba (Yoh. 14:2, 3). Ijara ya waovu: Jehanamu (Mt. 10:28) Jehanamu ya moto (Mt. 5:22) Ufufuo wa hukumu (Yoh. 5:29), Hukumu ya Jehanamu (Mt. 23:33) Dhambi ya milele (Mk. 3:29).

   Hivyo watu wanapokufa, hawapati ijara zao bali hubaki makaburini hadi Yesu atakapokuja kuwafufua na kuwapa ijara zao. (Yoh. 5: 28, 29, Uf. 22: 12, 1Thes. 4:13-17)

2. *Maelezo ya kisa cha tajiri na Lazaro ni ya kufikirika*

   Watu wanapokufa, miili yao huzikwa na pumzi hurudi ilikotoka. (Mh. 12: 7) Katika kisa, yanaonekana macho, kifua, kiu inayokatwa kwa tone lililo katika kidole, ulimi, ni mwili au roho? Hivi ni kifua cha Ibrahimu ndicho alikowekwa maskini au Ibrahimu mzima mzima alionekana? Ikiwa kila mtakatifu huwekwa kwenye kifua cha Ibrahimu, hivi Ibrahimu ana kifua chenye ukubwa gani hata kutosha kubeba watakatifu wote! Ibrahimu alikufa, vipi aonekane? Ukubwa wa shimo una utata: Ni jembamba kuruhusu watu waweze kuonana na kusemezana lakini lina kina kirefu hata mtu asiweze kuruka kutoka kwenye hadhi moja hadi nyingine.

   Mafundisho yatokanayo na mfano wa tajiri na maskini Lazaro

1. Mibaraka ya duniani kwa uhalisi wake siyo yakini ni ya kupita. Tajiri alikufa akaacha utajiri wake na maskini alikufa, akatengana na umaskini wake.
2. Walio matajiri huwajibika siyo tu kwa yale watendayo bali pia kwa yale wasiyofanya kwa utajiri wao. Huyu tajiri alikuwa mwema akaruhusu maskini kula makombo ya mezani pake, lakini alikuwa na nafasi ya kuinua hali ya maskini iwe bora zaidi, jambo ambalo hakufanya.
3. Maisha tuliyo nayo ndiyo nafasi pekee tuliyonayo kwa ajili ya maandalizi ya ufalme ujao. Angalia, iliombwa ruhusa aliyekufa apate nafasi ya kuwa hai kwa muda mfupi, lakini haikutolewa.
4. Uchoyo, na ubinafsi, matumizi mabaya ya utajiri humnyima mtu sifa ya kuurithi ufalme wa milele wa Mungu. Tajiri hakutengwa na Ibrahimu kwa kuwa alikuwa tajiri, bali kwa sababu

hakutumia utajiri wake kuwapunguzia maumivu wasio na mali.

5. Mafundisho ya Biblia yatosha kutufanya wenye hekima hata kupata wokovu. Kunyimwa ruhusa ya kwenda kuhubiri walio hai kulipewa maelezo kwamba walio hai wasipowasikiliza Musa na manabii nao watapotea.